

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## BARAZA LA MADAKTARI TANGANYIKA BARAZA LA FAMASI TANZANIA

### TAARIFA KWA UMMA

#### UFAPANUZI WA HOJA ZA WARAKA WA WAZI KWA MH. WAZIRI WA AFYA ULIOHUSU WANAFUNZI KUPEWA USAJILI KUTOA MATIBABU KABLA YA KUHITIMU

**DODOMA: 07 Februari, 2025**

Tarehe 7 Februari, 2025 Wizara ilipokea kwa njia ya mitandao ya kijamii waraka wa wazi ulioelekezwa kwa Mhe. Waziri wa Afya kuhusu kuwepo kwa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi kurejea nchini na kusajiliwa kutoa matibabu kabla ya kuhitimu mafunzo yao ya udaktari na ufamasia. Waraka umeeleza pia uwepo wa wanafunzi wanaoghushi taarifa kwa kushirikiana Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Madaktari (MCT) na Baraza la Famasia (PCT) ili kupata shahada na vibali vya kutolea huduma za afya bila kuwa na vigezo. Sambamba na hili pia Waraka unaelezea kushushwa kwa vigezo vya udahili kwa fani za Uuguzi, Ufamasia na Udaktari.

Mabaraza yanapenda kuujulisha umma kuwa, inafanyia kazi hoja za waraka husika, hata hivyo Mabaraza yanapenda kuuhakikishia umma kuwa wataalamu wanaotoa huduma nchini hulazimika kudahiliwa kwa vigezo vya mitaala iliyoidhinishwa na Mamlaka za ithibati na kusajiliwa na Mabaraza ya kitaaluma kabla ya kuruhusiwa kutoa huduma. Aidha, Mabaraza yanasimamia vigezo vya usajili vyenye kuwezesha waatalamu wake kukubalika Tanzania na nje kwenye soko la Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla.

Mabaraza ya Kitaaluma ya Udaktari, Ufamasia na Ukunga na Uuguzi yanafuata taratibu zilizoainishwa kwenye Sheria zinazosimamia taaluma hizo ili kuhakikisha kwamba wanataaluma wenye vigezo na umahiri unaohitajika pekee ndio wanaosajiliwa kutoa huduma kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Taratibu zinazozingatwa zinaongozwa na Sheria zilizoanzisha mabaraza husika kupitia vifungu husika (*Kifungu cha 20 (1)(a) na (b) cha Sheria ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Wataalamu Afya Shirikishi, Sura ya 152 na Kifungu cha 14 (1)(2) na 16 (1) (2) cha Sheria ya Famasia, Sura ya 311*).

Kulingana na Sheria tajwa vigezo vya usajili vinayataka Mabaraza kujiridhisha kwamba mwanataaluma wa Udaktari na Ufamasia amekidhi vigezo na kupata

shahada husika kutoka taasisi inayotambulika na Serikali vilevile awe amefanya mafunzo ya utarajali na amefaulu mtihani wa taaluma uliotungwa na Baraza husika. Mabaraza hukagua nyaraka mbalimbali zikiwemo cheti cha kuzaliwa, cheti cha kidato cha nne, cheti cha kidato cha sita/ cheti cha Stashahada pamoja na cheti cha shahada ya mwanataaluma husika. Kwa wahitimu kutoka nje ya nchi huwajibika kuwasilisha cheti cha utambuzi wa Shahada zao kutoka TCU. Muda wa mafunzo na maudhui ni moja ya vigezo vinavyozingatiwa na Mabaraza katika utambuzi wa shahada husika.

Mabaraza yanapenda kuwahakikishia wananchi kuwa yataendelea kusimamia taaluma husika kwa kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na Miongozo inafuatwa kuanzia hatua za udahili, usajili pamoja na kutoa leseni za kutolea huduma za afya kwa wanataaluma ili kulinda afya za Watanzania. Aidha, Mabaraza yataendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kubaini ukiukwaji wa taratibu wenye kuruhusu wahitimu wasio na vigezo kupewa usajili na leseni za kutolea huduma za afya na ikibainika, wahasika watachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa Sheria.

**Imetolewa na;**



Dkt. David Paul Mnzava  
**MSAJILI**  
**BARAZA LA MADAKTARI TANGANYIKA**



Godfrey Christopher Ngonela  
**Kny: MSAJILI**  
**BARAZA LA FAMASI TANZANIA**